

**TANZANYA BİRLEŞİK
CUMHURİYETİ
BÜYÜKELÇİLİĞİ
TÜRKİYE**



**UBALOZI WA
JUMHURI YA
MUUNGANO WA
TANZANIA,
UTURUKI**

TAARIFA KWA UMMA

FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NCHINI UTURUKI (*TÜRKİYE SCHOLARSHIPS*) KWA MWAKA 2026/2027

Januari 10, 2026, ANKARA,

Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uturuki unapenda kuujulisha umma wa Watanzania kwamba Serikali ya Jamhuri ya Uturuki imetangaza fursa za ufadhili wa masomo (*scholarships*) katika ngazi za Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Ufadhili huo unajumuisha ada ya masomo, posho ya kujikimu kwa mwezi, bima ya afya, tiketi ya ndege, udahili wa chuo na usajili wa kozi (*university and program placement*), utafiti, malazi na mafunzo ya lugha.

Aidha, taarifa zaidi kuhusu ufadhili huo ikiwemo sifa na taratibu za uombaji zinapatikana kupitia Tovuti (<https://turkiyeburslari.gov.tr>). Maombi yote kuhusu ufadhili huo yanafanyika kupitia tovuti tajwa kuanzia Januari 10, 2026 na mwisho wa kutuma maombi ni Februari 20, 2026.

Tanzania na Uturuki zina ushirikiano mzuri kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu, hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa fursa hizi katika kuimarisha umahiri wa rasilimaliwatu nchini, Ubalozi unatoa wito kwa Watanzania wenye sifa kujitokeza kwa wingi kuomba nafasi hizo.

**UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NCHINI
UTURUKI**